

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS-TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA KIGAMBONI

Simu: +255 22-2928468
Fax: +255 22-2928469
Barua pepe :info@kigamboni.go.tz
Tovuti :www.kigamboni.go.tz



S.L.P 36009,
KIGAMBONI,
DAR ES SALAAM,
17/09/2018

TANGAZO LA ZABUNI
NA. LGA/181/NCS/2018-19/01
UKODISHAJI WA ENEO LA HALMASHAURI YA
MANISPAA YA KIGAMBONI

1. Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni katika mwaka 2018/2019 inatangaza mtu/kampuni yenye nia ya kukodi eneo lililopo Kata ya Vijibweni lenye ukubwa wa SQM 60,284 sawa Ekali 14.88. Eneo hili lipo katika mchoro wa mipango miji TP DRG No. 1/677/791A (Vijibweni industrial area Kigamboni Municipal) ambalo limepata idhini tarehe 20/10/2017 na ramani ya Mipango miji Na. E160/40 au Registered plan Na. 98692
2. Kwa wenyenia ya kukodi/kupanga eneo wanakaribishwa kukagua na vitabu vya zabuni vinapatikana katika **ofisi ya Katibu wa Bodi ya Zabuni Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni** iliyopo eneo la Mjimwema, malipo ya maombi ni Tshs. 100,000/= (Laki moja tu) ambayo haitarudishwa
3. Zabuni zote ziwe na **nakala halisi (original)** na **nakala mbili za kudurufu** zinazofanana, zilizojazwa kwa usahihi na zilizowekwa kwenye bahasha isiyo na maandishi juu na kuandikwa Zabuni Na. **LGA/181/NCS/2018-19 "ZABUNI YA UKODISHAJI WA ENEO LA HALMASHAURI YA MANISPAA KIGAMBONI LILILOPO VIJIBWENI"**

4. Maombi yote yapelekwe kwa **Katibu wa Bodi ya Zabuni, Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni S.L.P 36009 Dar es salaam**
5. Siku ya mwisho ya kuwasilisha Zabuni ni Tarehe 01/10/2018 kabla ya **saa 04.00 asubuhi**. Zabuni zote zitafunguliwa hadharani **saa 04.30 asubuhi** siku hiyo hiyo baada ya kupokelewa, mbele ya wawakilishi wa waombaji wanaoamua kuhudhuria katika ufunguaji wa zabuni katika **Ofisi ya Manunuzi na Ugavi Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni**.
- 5 Zabuni zitakazochelewa, au sehemu ya zabuni, zabuni za kielektroniki, na zisizofunguliwa katika tukio la ufunguaji kwa hali yoyote ile zabuni hizo hazitakubaliwa kwa tathmini.

Arch. Ng'wilabuzu N. Ludigija
Mkurugenzi wa manispaa
Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni

